



Yesmark Tuition Services

**IDARA YA KISWAHILI**

**DES 2015**

**KARATASI 102/3: FASIHI**

**MUDA: SAA 2½**

**Jibu maswali manne. Swali la kwanza ni la lazima. Chagua maswali mengine matatu kutoka kwa maswali yanayofuatia. Usijibu maswali mawili kutoka kitabu kimoja.**

**SEHEMU A: ushairi**

**SWALI 1:**

Hakika siku ya leo, ni siku ya majivuno  
Basi pasiwe na choyo, na usonono  
Tulekezane yaliyo, unawiri Muungano.

Tuzisafisheni nyoyo, pasiwe na miguguno  
Yaongoke tutakayo, kusiwe na mabishano  
Mbegu hii tupandayo, ilete mema mavuno.

Tufungulie upeo, Mola usiye mfano  
Pa kitasa na komeo, tupite bila kinzano  
Tupitishie njia hiyo, pasina masongamano

Twakuomba uumbao, mkono vyanda vitano  
Tushikane hii leo, tuwe moja tangamano  
Tupendane kwa pumbao, hali na maridhiano

Aliye ana machukiyo, adui wa Muungano  
Naazibe masikiyo, asisikie maneno  
Kisha awe kibogoyo, asiwe na moja jino.

Ya Ilahi ujalie, huu wetu Muungano  
Nuru yake izagae, na nguvu za mapigano  
Hasidi mpe hakie, mateso yaso mfano.

Watamati komeleo, kuimba kwangu hukuno  
Nataka maendeleo, yasiyo na malumbano  
Daima tuwe ni ngao, palipo **msagurano**.

- (a) Toa kichwa cha shairi hili. (alama 2)
- (b) Shairi hili ni la bahari gani? Taja **mbili**. (alama 2)
- (c) Taja sifa **tano** za aina hii ya ushairi. (alama 5)
- (d) Andika ubeti wa pili kwa lugha nathari. (alama 3)
- (e) Eleza maana ya mshororo ufuatao: Pa kitasa na komeo, tupite bila kinzano. (alama 3)
- (f) Huku ukitoa mifano mitatu eleza uhuru wa ushairi katika shairi hili. (alama 3)
- (g) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika shairi. (alama 3)
- (i) Usonono :
- (ii) Vyanda:
- (iii) Msagurano:

### **SEHEMU B: FASIHI SIMULIZI**

#### **SWALI 2:**

- a) Eleza sifa za utani kama kipera cha mazungumzo katika fasihi simulizi. (Alama 4)
- b) Utani una umuhimu gani? (Alama 8)
- c) Onyesha changamoto zinazokabili kipera hiki cha utani. (Alama 8)

#### **SWALI 3:**

#### **Soma utungo ufuatao kasha ujibu maswali.**

Ni vigumu  
Aloo  
Ahaa.....  
Ni vigumu kuacha kwenu  
Kwenda kwingineko  
Ni vigumu kumwita mwingine  
Mama yako  
Baba alielimishwa kule

Na ni karani  
Nimemuona karani  
Nimemuona karani  
Mlinzi wetu ni karani  
Mama alielimishwa  
Na ni muuguzi  
Mama alitaka  
Mama alitaka mwanawe  
Awe muuguzi  
Lima shamba la matunda  
Lima mama shamba la matunda  
Ndipo yastawi na kuzaa  
Aloo!  
Aha! Aha!

**Maswali**

- (a) Tambua aina ya wimbo huu. (alama 2)  
(b) Fafanua maudhui yaliyomo katika wimbo huu. (alama 6)  
(c) Eleza sifa sita zinazohusishwa na wimbo wa aina hii. (alama 6)  
(d) Nyimbo za aina hii zilikuwa na umuhimu gani? (alama 6)

**SEHEMU C: utengano ( SAID A. MOHAMED)**

**SWALI 4:**

“Na juu ya ila hizo alizokuwa nazo, alichukua ujuba na ufedhuli. Wanasema mwanamke huyu kanywa maji ya chooni.”

- a) Fafanua muktadha wa maneno haya. (Al. 4)  
b) Tambua tamathali iliyotumika katika dondoo hili. (Al. 2)  
c) Zitaje ‘ila hizo alizokuwa nazo’. (Al. 4)  
d) Huku ukitoa mifano maridhawa, fafanua **HOJA TANO** kudhihirisha uozo wa jamii katika riwaya nzima. (Al. 10)

**SWALI 5:**

Eleza kwa tafsili jinsi ukwepaji wa majukumu unavyojitokeza katika Riwaya ya Utengano. (Al. 20)

**SEHEMU D: DAMU NYEUSI NA HADITHI NYINGINE (KEN WALIBORA NA SAID A. MOHAMED)**

**SWALI 6.**

Jadili ufaafu wa anwani ‘Damu Nyeusi’ katika hadithi ya Damu nyeusi na ken Walibora.  
(Al 20)

**SWALI 5.**

“Badala ya kujihisi salama, niliingiwa na wazo la kuwa debe tupu.”

- a) Weka dondoo hili katika muktadha wake. (al.4)
- b) Ni tamathali gani ya usemi iliyotumika kwenye dondoo.
- c) Bainisha sifa za mhusika anayerejelewa kweye dondoo. (al.4)

**SEHEMU E: MUSTAHIKI MEYA (TIMOTHY M. AREGE)**

**SWALI 6.**

Jadili maudhui ya Sera mbovu za kiuchumi kama yaliyosawiriwa kwenye tamthilia ya mstahiki meya.  
(Alama 20)

**SWALI 7.**

‘Ni furaha yangu kuona wanasiasa kama wewe wakiufuata upendo wa Bwana.’

- a) Bainisha muktadha iliyotumika kauli hii. (alama 4)
- b) Kauli hii inadhihirisha matumizi ya mbinu ipi ya lugha? Fafanua (alama 4)
- c) Jadili sifa zozote mbili za mnenaji kulingana na muktadha huu (alama 4)
- d) Bainisha sifa zozote nne za mnenewa kulingana na muktadha huu (alama 8)